JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

MWONGOZO WA MTUMIAJI WA MFUMO WA KURA YA RAIS PORTAL (KRP)

Anwani ya Simu: *"UCHAGUZI"*

Nambari ya Simu: *+255 26-2962345-8*

Nambari ya Nukushi: *+255 26-2962348*

Baruapepe: *uchaguzi@inec.go.tz*

Tovuti: *www.inec.go.tz*

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi,

Uchaguzi House,

Eneo la Uwekezaji Njedengwa,

Kitalu D, Kiwanja Na. 4,

5 Barabara ya Uchaguzi,

S.L.P 358,

41107 DODOMA.

Agosti, 2025

1. Utangulizi

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imesanifu na kujenga mfumo unaowezesha Mpiga Kura kupiga kura ya Rais tofauti na kituo alichojiandikisha. Maombi haya yanaweza kuanzishwa na Mpiga Kura mwenyewe, ama kupitia kwa Msimamizi wa Uchaguzi katika jimbo husika.

Mfumo huu una watumiaji wa aina tatu:

- Mpiga Kura
- Msimamizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo (RO)
- Muidhinishaji(Approver).

2. Mpiga Kura

2.1. Maombi Yanayowekwa na Mpiga Kura Mwenyewe (Self Applications)

2.1.1. Mpiga Kura Aliyeandikishwa na INEC

i. Mpiga Kura atajaza Namba ya Utambulisho wa Taifa (NIN) pamoja na Namba ya Mpiga Kura (Voter ID),

ii. kisha atatakiwa kujibu maswali 5 ikiwa ni hatua ya uhakiki wa taarifa na utambuzi (Identification and Verification). Ikiwa Mpiga Kura atajibu maswali kwa usahihi ataelekezwa kuweka Namba ya Simu ambayo itapokea Namba ya Siri ya Mara Moja (OTP).

iii. Mpiga Kura atatakiwa kuingiza namba hiyo kwa usahihi kisha kubonyeza kitufe kilichoandikwa “TUMA”.

iv. Mpiga Kura atatakiwa kujaza taarifa za Kituo anachotarajia kupigia kura. Taarifa hizo zinajumuisha Mkoa, Halmashauri, Jimbo, Kata/Shehia, Kituo cha Kupigia Kura, pamoja na sababu ya kuomba kupigia kura katika kituo hicho.

v. Mpiga Kura atakapobofya kitufe cha “TUMA” atapokea ujumbe wa papo kwa papo katika *screen* yake, na ujumbe mfupi wa maandishi SMS katika simu yake kupitia namba aliyotumia katika ombi husika. Ujumbe utamjulisha kufanikiwa kutuma ombi la kuhamisha taarifa za kituo cha kupigia kura, na kufahamishwa kuwa baada ya Uhakiki atapokea SMS juu ya ombi lake.


Hongera
Ndugu Mpiga Kura
Hongera umefanikiwa kutuma maombi yako yenye KUMB NA. PPT1000265, utapokea ujumbe mfupi baada ya uhakiki wa maombi yako kukamilika
Maelezo muhimu kwa Mpig
Tafadhali chagua utambulisho wako
NIDA
ZAN ID
Ingiza namba ya NIDA
Ingiza namba ya Mpiga kura (INEC)
TUMA
© 2025 INEC
Kanusho

2.1.2. Mpiga Kura Aliyeandikishwa na ZEC (Self Application)

i. Mpiga Kura atajaza Namba ya Utambulisho wa Mzanzibar Mkaazi (ZAN ID).



ii. Kisha atatakiwa kujibu maswali 5 ikiwa ni hatua ya uhakiki wa taarifa na utambuzi (Identification and Verification).



Ikiwa Mpiga Kura atajibu maswali kwa usahihi ataelekezwa kuweka Namba ya Simu ambayo itapokea Namba ya Siri ya Mara Moja (OTP).



iii. Mpiga Kura atatakiwa kuingiza namba ya siri aliyopokea kwa usahihi kisha kubonyeza kitufe kilichoandikwa “TUMA”.



iv. Mpiga Kura atatakiwa kujaza taarifa za Kituo anachotarajia kupigia kura. Taarifa hizo zinajumuisha Mkoa, Halmashauri, Jimbo, Kata/Shehia, Kituo cha Kupigia Kura, pamoja na sababu ya kuomba kupigia kura katika kituo hicho.



v. Mpiga Kura atakapobofya kitufe cha “TUMA” atapokea ujumbe wa papo kwa papo katika skrini yake, na ujumbe mfupi wa maandishi SMS katika simu yake kupitia namba aliyotumia katika ombi husika. Ujumbe utamjulisha kufanikiwa kutuma ombi la kuhamisha taarifa za kituo cha kupigia kura, na kufahamishwa kuwa baada ya Uhakiki atapokea SMS juu ya ombi lake.



3. Msimamizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo

i. Msimamizi wa Uchaguzi ataingia kwenye Mfumo wa KRP kwa kuweka Jina la mtumiaji na nywila(nenosiri) (Username na Password).



ii. Msimamizi wa Uchaguzi atakapofanikiwa kuingia katika mfumo ataona menu Maombi, Daftari.

iii. Katika menu ya maombi ina Zilizotumwa, Zilizokubaliwa, Zilizokataliwa, Maombi Mtandao.

Msimamizi anaweza kuanzisha ombi kwa kubofya “Anza ombi jipya”



iv. Kisha atachagua kutumia Namba ya Mpiga Kura kama alivyoandikishwa INEC au ZEC kisha atabofya kitufe kilichoandikwa “TUMA”





v. Mfumo utafunguka ukurasa unaoonyesha taarifa za Mpiga Kura kwa kutumia namba ya mpiga kura.



vi. Msimamizi wa Uchaguzi atabofya kitufe kilichoandikwa “ENDELEA” na atajaza taarifa za kituo anachotarajia kupigia kura.



vii. Msimamizi wa Uchaguzi atatakiwa kupakia Fomu Na. 29 iliyojazwa na Mpiga Kura.



viii. Msimamizi wa Uchaguzi atakapobofya kitufe cha “TUMA” atapata ujumbe wa papo kwa papo (popup) ikionesha kufanikiwa kutumwa kwa Ombi la Mpiga Kura kupitia kwa Msimamizi wa Uchaguzi, na Mpiga Kura atapokea SMS ikionesha kufanikiwa kutuma ombi la kuhamisha taarifa za kituo cha Kupigia Kura akitakiwa kusubiri maamuzi ya Ombi lake baada ya Uhakiki.



ix. Msimamizi wa Uchaguzi ataweza Kupakua Orodha za Wapiga Kura walioomba kupigia Kura katika vituo tofauti na walivyoandikishwa, pia ataweza kupakua orodha ya Wapiga Kura walioomba kuhamishia taarifa zao za vituo vya Kupigia katika maeneo mengine.

4. Masuala ya Kiufundi na Vidokezo

- Hakikisha unaunganisha kifaa chako na mtandao wa kuaminika
- Tumia jina sahihi la mtumiaji na nywila ulizopewa na ubadishe nywila yako ambayo utaitumia wewe tuu
- Mpiga Kura atahitajika kufahamu taarifa zake kwa usahihi kama zilivyo katika kanzidata za serikali
- Mpiga Kura anahimizwa kutunza taarifa zake katika sehemu salama